TANGAZO LA SERIKALI NA. 227 la tarehe 4/4/2025

SHERIA YA MISITU,
(SURA YA 323)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 106(1)(aa))*

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA UTARATIBU WA USAFIRISHAJI WA VENIA KWENDA NJE YA NCHI ZA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 807 la 2024

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Utaratibu wa Usafirishaji wa Venia Kwenda Nje ya Nchi za Mwaka 2025 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Utaratibu wa Usafirishaji wa Venia Kwenda Nje ya Nchi za Mwaka 2024, ambazo hapa zinarejewa kama “Kanuni kuu”.

Marekebisho ya kanuni ya 5

2. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 5 kwa-

(a) kuongeza maneno “ndani ya siku saba” baada ya neno “Uhifadhi” lililopo katika kanuni ndogo ya (1); na
(b) kufuta maneno “kanuni ndogo ya (1)” yaliyopo katika kanuni ndogo ya (4) na badala yake kuweka maneno “kanuni ndogo ya (3), ndani ya siku kumi na nne”.

Marekebisho ya kanuni ya 9

3. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 9 kwa kuongeza mara baada ya kanuni ndogo ya (2) kanuni ndogo mpya ifuatayo:

"(3) Bila kuathiri masharti ya kanuni hii, maombi yote yaliyopokelewa kabla ya tarehe ya mwisho ya matumizi ya Kanuni hizi yataendelea kufanyiwa kazi hadi yatakapokamilika.

Dodoma,
26 Machi, 2025

PINDI HAZARA CHANA
*Waziri wa Maliasili na Utalii*